## MASHAIRI

*Kineene wa Mutiso*

**SINILETEE SIASA**

1. Nali na njaa hatari, nami sipendi vya wizi,
   Nikamwendea tajiri, kutaka usaidizi,
   Nikampasha habari, sijala karibu mwezi,
   Kanifokea vikali, siniletee siasa!!!

2. Mwajiri nikamwendea, kumwomba anipe kazi,
   Mavyeti kampatia, ya kazi na ya ujuzi
   Mawazo yakanijia, kanidondoka machozi,
   Mwajiri kanirukia, , ondoka sina maziwa!!!

3. Nilipotoka afisi, nende kwa yangu makazi,
   Ukanipata mkosi, kapigwa na majambazi,
   Nikaripoti polisi, huku nalia machozi,
   Polisi wakanikanya, 'hliwo ndiwo uchochezi'.

**UNAFIKI W A DINI.**

1. Bwanyenye, kwenda kanisa, huku alindwa vikali,
   Bwanyenye, kusoma misa, naye ni kupe katili,
   Bwanyenye, kumwiga Mussa, na wana wa 'Siraeli,
   Mwasema si unafiki?!

2. Bwanyenye, kihalalisha, maovu kwa *Biblia,*
   Bwanyenye, akifundisha, usawa wa insia,
   Bwanyenye, kuwakilisha, ambao awachukia,
   Hamwoni ni unafiki?!

3. Bepari, Kirisimasi, Mwokozi kumkumbuka,
   Bepari, kuwa kasisi, imamu na kadhalika,
   Bepari, kuwa ja sisi, wanyonge tulonyongeka,
   Ndu zangu si unafiki?!

4. Dini, kutounganisha, wanyonge na matajiri,
   Dini, kutofundisha, tujionee fahari,
   Dini, kutukengeusha, kwa lugha iso dhahiri,
   Wangapi wataamini?!

## VIONGOZI

1. Raisi, kuwa katili, ni nduli mchinja watu,
   Raisi, kuwa bahili, amiliki kila kitu,
   Raisi, kuwa jahili, avaliwa ja viatu,
   Raisi, kiiga Wazungu, wanyonge huiga nani?!

2. Waziri, mwizi akiwa, na kuwaiga wageni,
   Waziri, hongo kipewa, awe tajiri nyumbani,
   Waziri, kuheshimiwa, hasemi na watu duni,
   Waziri, kinyonya raia, wanyonge nawanyamaze?!

3. Wabunge, wakipigana, wakivunjana ja punda,
   Wabunge, wakiwindana, mithili kuku na nunda,
   Wabunge, kivunja sana, sheria wanazounda,
   Wabunge, kijiwakilisha, wanyonge nawanyamaze?!

4. Hakimu, hongo kipewa, pasi sababu unyongwe,
   Hakimu, kiamriwa, msi niakosa afungwe,
   Hakimu, akisifiwa, kwa kuwanyonga vikongwe,
   Hakimu, akiwa Mzungu, weusi nawanyamaze?!

5. Tabibu, kiamriwa, Ulla wazimu aserne,
   Tabibu, unauguwa, matibabu akunyime,
   Tabibu, pesa kupewa, ataka na akukame,
   Tabibu, akiuwa watu, wagonjwa nawanyamaze?!

6. Wageni, kututawala, sheriya kututungia,
   Wageni, kula mahala, wenyeji kututumia,
   Wageni, na zetu mila, zote kutuharibia,
   Wageni, wakituongoza, wenyeji nawanyamaze?

7. Tajiri, akimhonga, mkubwa kama polisi,
   Tajiri, duka kifunga, illi atese unasi,
   Tajiri, akijibwanga, nakutuita mafisi,
   Tajiri, akiwa languzi, wanyonge nawanyamaze?

8. Wazazi, kuwa idhaa, daima wanagombana,
   Wazazi, siri kitoa, na wote kusengenyana,
   Wazazi, wakifikia, hatua ya kupigana,
   Wazazi, wanapopigana, watoto hufanya nini?

9. Walimu, kuwa wajinga, wafunzwe na wafunzao,
Walimu, wakiwatwanga, mchana kutwakilio,
Walimu, wakiwapinga, wanafu pasi kiao,
Walimu, kifanya ghasiya, wanafu hufanya nini?

10. Shetwani, Mungu kumwasi, na Mungu alla uwezo,
Shetwani, kuitwa Lusi, na swifa nyingi ja hizo,
Shetwani, kuwa Raisi, kwa malaika ni nguzo,
Shetwani, kumshinda Mungu, hawaa si ni mswaki?!

11. Chuo, Kikuu kijenga, waruhusiwao nani?
Chuo, Kikuu kipinga, wenyi elimu ni nyani?
Chuo, Kikuu kifunga, na shule mwajenga zani?
Chuo, Kikuu kioza, na shule zitakuwaje?!

12. Polisi, kiamriwa, apige pasi sababu,
Polisi, kinunuliwa, burre akupe adhabu,
Polisi, kiruhusiwa, apake watu aibu,
Polisi, wakitunyang' anya, wanyonge natunyamaze?!

**BADO**

1. Bado, mnatunyonya, twavumiliya uchungu,
Bado, mwatunyang'anya, kisingizia Mzungu,
Bado, mnajifanya, eti mwancha Mungu!

2. Bado, ninazunguka, kula afisi mefika,
Bado, na sijachoka, ijapo minne miaka,
Bado, nasononeka, nguo viraka naweka.

3. Bado, sinayo kazi, ijapo nimehitimu,
Bado, yangu mavazi, ndio mizani muhimu,
Bado, yasema mwizi, jambazi lilohitimu.

4. Bado, ningali naja, katika hini afisi,
Bado, nnayo haja, nataka kumwona bosi,
Bado, saga nangoja, nipate hiyo nafasi.

5. Bado, nna harani, macho ya mheshimiwa,
Bado, yuko kazini, angali anikaguwa,
Bado, ashikakaru, ondoka watusumbuwa.

6. Bado, nnasimama, naunda yangu plani,
Bado, kimwana mafia, chanitazama ja nyani,
Bado, kina tuhuma, najua shule ni nini.

7. Bado, wageni waja, Wazungu, Wahindi, hawa,
Bado, wangia ndani, pasipo kuzuiliwa,
Bado, ni *waniwani,* na hongo bosi kupewa.

8. Bado, twasisitiza, mvae tai na suti,
Bado, tunawajuza, twataka watanashati,
Bado, tunakataza, kujiwa pasi *ripoti.*

9. Bado, hujafahamu, vyetivyo hatuvitaki,
Bado, ewe sanamu, kutusumbua huchoki,
Bado, u mahamumu, na hapa hatuwataki.

10. Bado, haujakamwa, ngoja askari waja,
Bado, haujazimwa, *spidi* hizo za luja,
Bado, haujapimwa, mifupa ya kilo moja.

11. Bado, haujasoma, na hapa tuna walimu,
Bado, una ukoma, na dawa ziko muhimu,
Bado, hufanyi hima, ukaondoka hasimu?!

12. Bado, hujaelewa, afisi hii si yako?
Bado, wajizuzuwa, twataka taabu zako,
Bado, hujaambiwa, ya kwamba kazi haiko?

13. Bado, haujasoma, kibao kilicho wazi,
Bado, kipo chasema, RUDI HAKUNA KAZI,
Bado, hujanikoma, na hiyo yako kutuzi.

14. Bado, hujakubali, mwito wa Raisi wetu,
Bado, na serikali, yataka zaraa yetu,
Bado, wataka mali, kwa kuwaibia walli.

15. Bado, ninakuonya, sirudi hapa kitwana,
Bado, wajidanganya, *bosie* utamuona,
Bado, haujamanya, *bosie* si yako nana?